JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII,
JINSIA, WAZEE NA WATOTO



HADIDU ZA REJEA ZA KAMATI YA UHAKIKI WA VIELELEZO VYA ELIMU YA AFYA KWA UMMA NCHINI

IDARA YA KINGA
KITENGO CHA ELIMU YA AFYA KWA UMMA
MACHI, 2021

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO

HADIDU ZA REJEA ZA KAMATI YA UHAKIKI WA VIELELEZO VYAELIMU YA AFYA KWA UMMA NCHINI

IDARA YA KINGA - KITENGO CHA ELIMU YA AFYA KWA UMMA

MACHI, 2021

Yaliyomo

Dibaji v
Shukrani vi
SEHEMU YA KWANZA: UTANGULIZI 1
SEHEMU YA PILI: WAJUMBE WA KAMATI YA UHAKIKI WA VIELELEZO 3
2.1 Sifa za wajumbe wa Kamati ya uhakiki wa vielelezo ... 3
2.2 Wajumbe wa Kudumu..... 3
2.3 Wajumbe wa Kualikwa 5
2.4 Sekretarieti 5
2.5 Uteuzi wa wajumbe wa Kamati 5
2.6 Ukomo wa kuwa mjumbe wa Kamati 6
2.7 Uongozi wa Kamati 6

SEHEMU YA TATU: DHUMUNI NA MAJUKUMU YA KAMATI YA UHAKIKI WA VIELELEZO 7
3.1 Dhumuni 7
3.2 Majukumu 7

SEHEMU YA NNE: VIKAO VYA KAMATI YA UHAKIKI WA VIELELEZO 9
4.1 Vikao vya Kawaida 9
4.2 Vikao vya Dharura 10
4.3 Vikao vya Tathmini 10

SEHEMU YA TANO: NYENZO NA GHARAMA ZA UHAKIKI WA VIELELEZO..... 11
5.1 Nyenzo ya kupitia na kuhakiki vielelezo 11
5.2 Gharama za vikao vya uhakiki 11

SEHEMU YA SITA: HITIMISHO 12

Dibaji

Elimu ya Afya kwa Umma ni muhimu katika kuhakikisha jamii inakuwa na uelewa wa namna nzuri ya kujikinga na magonjwa mbalimbali. Suala la kuelimisha jamii kuhusu afya ni jambo linalotakiwa kufanywa kwa ushirikiano mkubwa kati ya Serikali, Wadau na Taasisi washirika.

Ili kufikia lengo hili ni muhimu kuwepo na Kamati ya wataalam wenye utaalam wa kuhakikisha kuwa elimu ya afya inayotolewa kwa jamii ina ubora na viwango kulingana na Miongozo ya uelimishaji, uhamasishaji na ushirikishaji jamii. Kamati hii ni sharti izingatie kuwa elimu kusudiwa pamoja na njia pendekezwa kufikisha elimu kwa umma ina ubora unaokidhi na kuzingatia viwango vya kitaaluma; mila, desturi na tamaduni, pamoja na kanuni na sheria za nchi. Lengo hasa ni kuhakikisha kuwa ujumbe unaofikishwa ni sahihi kwa hadhira sahihi na kwa wakati sahihi.

Wizara ya Afya, Maendeleo ya jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ndiyo yenye dhamana ya kuteua Kamati yenye weledi mzuri ili kuhakikisha jamii inapatiwa ujumbe mahususi wa Afya katika kuboresha na kustawisha Afya ya jamii.

Kamati hii itafanya kazi kwa mujibu wa Miongozo iliyopo ili kuhakikisha kuwa shughuli za uelimishaji jamii zinafanywa kwa ufanisi. Katika kutimiza jukumu hili, Kamati itahakikisha kuwa mila na desturi, utu, tamaduni na maadili ya nchi yanalindwa katika nyaraka mbalimbali zitakazoandaliwa na kutumiwa na Wadau katika kutoa Elimu ya Afya kwa Umma.

Prof. Mabula D. Mchembe
KATIBU MKUU (AFYA)

Shukrani

Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii Jinsia Wazee na Watoto inapenda kutambua na kuwashukuru Wadau mbalimbali kwa mchango wao wa kufanikisha uandaaji wa Mwongozo huu ambao utasaidia kurahisisha kazi za Kamati katika kupitia na kuhakiki vielelezo vya utoaji wa Elimu ya Afya nchini.

Kipekee niwashukuru wafanyakazi wa Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto (WAMJW), Idara ya Kinga chini ya uongozi wa Mkurugenzi Dkt. Leonard Subi kwa usimamizi mzuri. Zaidi nimshukuru Kaimu Mkurugenzi Msaidizi wa Kitengo cha Elimu ya Afya kwa Umma Dkt. Amalberga Kasangala kwa kusimamia na kuongoza wataalam walioshiriki kuandaa Mwongozo huu. Wizara inapenda pia kutambua ushiriki wa Idara mbalimbali za Wizara kwa mchango wao wa hali, mali na ujuzi kufanikisha ukamilishaji wa Mwongozo huu.

Aidha, napenda kuwatambua wafuatao kwa mchango wao wa kufanikisha kukamilika kwa Mwongozo wa Hadidu za Rejea kwa ajili ya Kamati ya Uhakiki wa Vielelezo vya Elimu ya Afya nchini. Watu hao ni pamoja na Dr. Adeline Kimambo (Mshauri wa kujitegemea katika masuala ya Mawasiliano), Bw. Dereck Murusuli (Kamati ya Maudhui, Mamlaka ya Mawasiliano nchini), Bw. Isaack Kitururu (Mshauri wa Kujitegemea), na Bw. Romanusi Tairo (Bodi ya Filamu). Wengine ni Bw. Peter Mabwe, Bw. Ismail Hamidu na Bw. Simon Nzilibili kutoka Kitengo cha Elimu ya Afya kwa Umma.

Hali kadhalika, nashukuru Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) kwa kujitoa kwao bila kuchoka kukamilisha uandaaji wa Mwongozo huu.

Kwa kuzingatia dhana ya ushirikishwaji wa Wadau, Wizara inapenda kushukuru na kutambua mchango wa Wadau wote walioshiriki katika kazi hii.

Prof. Abel Makubi
MGANGA MKUU WA SERIKALI

SEHEMU YA KWANZA: UTANGULIZI

Elimu ya afya kwa umma ni jambo la msingi sana ili kuhakikisha jamii inakuwa na uelewa wa masuala mbalimbali yahusuyo afya na hatimaye kujikinga na maradhi. Ni wazi kwamba pale jamii inapoelimishwa vizuri na kisha kuzingatia kanuni za afya katika maisha itaipunguzia Serikali gharama kubwa za kupambana na maradhi. Aidha, elimu hii huongeza mbinu za kujikinga kwa jamii husika na hivyo muda wote kuwa na jamii yenye afya tayari kwa kushiriki katika shughuli za kiuchumi.

Kwa sasa shughuli ya utoaji elimu ya afya kwa umma imekuwa ikifanywa na Wadau mbalimbali kuanzia Serikali kuu, Serikali za Mitaa, Wadau wa Maendeleo, Mashirika ya Umma, Asasi za Kidini na za Kijamii.

Aidha, Wadau hao wamekuwa wakitumia mbinu, mifumo na njia mbalimbali kuhakikisha wanaelimisha jamii kuhusu umuhimu wa kuwa na afya bora. Miongoni mwa njia hizo ni pamoja na machapisho, mabango, vipeperushi, nyimbo, ujumbe mfupi wa simu, ikiwa ni mifano michache. Kwa nyenzo na njia yoyote inayotumika, elimu hii inapaswa kuwa sahihi, kwa rika sahihi na kwa wakati sahihi.

Ujumbe kutoka kwa Wadau umekua ukipitiwa na kuhakikiwa na timu ya wataalam kutoka kitengo cha Elimu ya Afya kwa Umma pekee. Ili kuongeza utaalam na ushirikishwaji ni vema kuongeza wajumbe kutoka Taasisi na Idara zingine kwa ufanisi zaidi.

Hata hivyo, Wizara ya Afya, Maendeleo ya jamii, Jinsia, Wazee na Watoto (WAMJW) kupitia Idara ya Kinga, Kitengo

cha Elimu ya Afya kwa Umma ndiyo yenye dhamana ya kuhakikisha kuwa vielelezo vyote vinavyoandaliwa kwa ajili ya kutoa elimu ya afya kwa umma vinazingatia siyo tu maadili ya Mtanzania bali pia kuwa na ubora mahususi na vyenye ujumbe unaoeleweka kabla ya vielelezo hivyo havijasambazwa kwa matumizi ya jamii.

Kwa kutambua umuhimu wa jukumu hili, WAMJW kupitia Kitengo cha Elimu ya Afya kwa Umma imeona kuna umuhimu wa kuimarisha Kamati itakayokuwa na jukumu la kupitia na kuhakiki vielelezo vyote vinavyoandaliwa na Wadau mbalimbali kwa ajili ya kutoa elimu ya afya kwa umma inayolenga mabadiliko ya tabia (SBCC Content Review Committee) ambayo itasimamiwa moja kwa moja na WAMJW.

SEHEMU YA PILI: WAJUMBE WA KAMATI YA UHAKIKI WA VIELELEZO

Kamati ya uhakiki vielelezo itaundwa na aina mbili za wajumbe, wajumbe wa kudumu na wajumbe wa kualikwa.

2.1 Sifa za wajumbe wa Kamati ya uhakiki wa vielelezo

a) Uelewa ama uzoefu katika taaluma, sera, sheria, taratibu kuhusiana na masuala ya uelimishaji na uhamasishaji unaolenga mabadiliko chanya ya mila, desturi na tabia zinazohusu masuala ya afya.
b) Utayari wa kuhudhuria vikao vya Kamati kwa mujibu wa Kalenda na ilivyoelekezwa
c) Utayari wa kushauri mambo muhimu yanayohusu Sera ya Afya
d) Utayari wa kupokea na kutekeleza kwa weledi na uadilifu majukumu ya Kamati
e) Kuweka wazi mgongano wa kimaslahi na waandaaji wa vielelezo vya kuelimisha jamii ambao unaweza kuathiri utekelezaji wa majukumu au maamuzi yake kwenye Kamati

2.2 Wajumbe wa Kudumu

Wajumbe wa kudumu watakuwa tisa (9) na watatoka katika Wizara na Taasisi za Serikali pamoja na Asasi zisizo za Kiserikali. Wajumbe hawa wanaingia kutokana na nafasi na weledi wao katika masuala ya kuelimisha na kuhamasisha jamii.

Wajumbe wa kudumu wa Kamati ya Uhakiki wa Vielelezo vya Elimu ya Afya kwa Umma

Na.	Mhusika	Majukumu
1	Mkurugenzi Kitengo cha Sheria, WAMJW	Kutoa ushauri wa kisheria
2	Mkurugenzi Kitengo cha Mawasiliano Serikalini, WAMJW	Kutoa ushauri na utaalam kuhusu masuala ya mawasiliano.
3	Mkurugenzi Msaidizi Elimu ya Afya kwa Umma, WAMJW	Kuratibu masuala ya Uelimishaji na Uhamasishaji
4	Wajumbe kutoka Taasisi za Elimu na Vyuo Vikuu • Mtaalam wa Sayansi za Elimu ya Jamii, Mwitiko Mawasiliano	Kutoa ushauri kuhusu masuala ya mabadiliko ya tabia na Saikolojia
	• Sayansi ya Tabia na mabadiliko ya Tabia jamii	Kutoa ushauri kuhusu masuala ya elimu ya afya katika jamii
	• Mtaalam wa Habari na Mawasiliano ya Umma	Kutoa ushauri kuhusu njia muafaka ya kufikisha ujumbe kutumia vyombo vya Habari
5	Mjumbe kutoka Bodi ya Filamu Tanzania	Kutoa ushauri kuhusu masuala ya picha-jongevu na taratibu za nchi katika uhakiki wa vielelezo vya uelimishaji.
6	Mjumbe kutoka (OR-TAMISEMI)	Kutoa ushauri kuhusu masuala ya utendaji na uratibu katika ngazi ya Serikali za Mitaa na jamii
7	Mjumbe kutoka Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA)	Kutoa ushauri kuhusu Miongozo na taratibu za mawasiliano nchini

2.3 Wajumbe wa Kualikwa

Kamati itakuwa huru kujumuisha wajumbe wa kualikwa kulingana na vielelezo vinavyohakikiwa. Vigezo vya ushiriki wa wajumbe hawa wa kualikwa vitategemea utaalam wa mjumbe au umuhimu wa Taasisi au kikundi cha kijamii katika vielelezo vilivyowasilishwa. Ushiriki wao utazingatia:-

a) Uwakilishi wa Idara au Taasisi kulingana na mahitaji au vielelezo vilivyowasilishwa
b) Mahitaji ya Kamati kwa wakati huo.

2.4 Sekretarieti

Sekretarieti itaundwa na baadhi ya watumishi kutoka Kitengo cha Elimu ya Afya kwa Umma ikiongozwa na Katibu wa Kamati. Sekretarieti itajumuisha;

a) Mratibu wa Kamati ya Uhakiki wa Vielelezo vya Elimu ya Afya kwa Umma
b) Waratibu wa programu zilizo chini ya Kitengo cha Elimu ya Afya kwa Umma ambao ni;
    i) Mratibu wa Programu ya Mawasiliano ya Afya na Mabadiliko ya Tabia Jamii (HC-SBBC)
    ii) Mratibu wa Programu ya Huduma za Afya ngazi ya Jamii (CBHP)
    iii) Mratibu wa Programu ya Afya Shuleni (NSHP)

2.5 Uteuzi wa wajumbe wa Kamati

a) Wajumbe watapendekezwa na Wizara ama Taasisi za Serikali kulingana na mahitaji.
b) Uteuzi rasmi wa wajumbe wa Kamati utafanywa na Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto baada ya kupokea mapendekezo kutoka Wizarani au Taasisi husika.

c) Uteuzi wa wajumbe utadumu kwa kipindi cha miaka mitatu. Mjumbe anaweza kuteuliwa tena kutokana na ufanisi wake ndani ya Kamati au mapendekezo ya Taasisi yake.

2.6 Ukomo wa kuwa mjumbe wa Kamati

a) Kumaliza muda wake
b) Kujiuzulu
c) Kuhama au kukoma kwa utumishi kwenye Taasisi anayoiwakilisha
d) Kutohudhuria vikao vitatu mfululizo bila taarifa
e) Ugonjwa wa muda mrefu unaopelekea Mjumbe kushindwa kutekeleza majukumu
f) Kifo

2.7 Uongozi wa Kamati

a) Mwenyekiti wa Kamati atateuliwa na Katibu Mkuu wa Wizara kutoka miongoni mwa wajumbe wa Kamati wanaotoka nje ya WAMJW
b) Katibu wa Kamati atateuliwa na Katibu Mkuu wa Wizara kutoka miongoni mwa wajumbe ambao ni watendaji wa Idara ya Kinga, kitengo cha Elimu ya Afya kwa Umma

SEHEMU YA TATU: DHUMUNI NA MAJUKUMU YA KAMATI YA UHAKIKI WA VIELELEZO

3.1 Dhumuni

Kuimarisha na kuongeza Ubora wa vielelezo vya elimu ya afya nchini na kuhakikisha kuwa ujumbe unaofikishwa unazingatia viwango vya kitaaluma; mila, desturi na tamaduni, pamoja na sheria na kanuni za nchi.

3.2 Majukumu

Kamati itatekeleza wajibu wake wa kupitia na kuhakiki vielelezo vya elimu ya afya kwa umma kwa kupitia majukumu yafuatayo;

a) Kupokea taarifa fupi kutoka Sekretarieti kuhusu vilelezo vilivyowasilishwa Wizara ya Afya kwa ajili ya uhakiki
b) Kupitia taarifa ya kila Mdau aliyewasilisha vielelezo/ kielelezo Wizara ya Afya kwa ajili ya uhakiki. Kazi hii itafanywa kwa kutumia fomu ya uhakiki.
c) Kuhakiki vielelezo na kuushauri Uongozi wa Wizara kuhusu kuidhinisha matumizi ya vielelezo vinavyokidhi viwango vya ubora au kutoidhinisha matumizi ya vielelezo ambavyo havikidhi viwango.
d) Kushauri Sekretarieti namna ya kuboresha ufanisi na kutatua migogoro inayohusu uandaaji wa vielelezo na watumiaji/walengwa wa vielelezo (jamii).
e) Kutoa ushauri wa kitaalam kwa Wadau wa elimu ya afya katika hatua zote za usanifu na uandaaji wa vielelezo kulingana na mahitaji.
f) Kuishauri Wizara kuhusu Miongozo ya kisheria, kisera, kanuni, vitendea kazi na mikakati ya kuinua kiwango cha ubora wa huduma za elimu ya afya nchini.

g) Kuhakikisha vielelezo vinavyotumika katika jamii vinalinda utamaduni wa Mtanzania na vinazingatia maadili ya taifa.
h) Kufanya ufuatiliaji wa ubora, uhalali na matumizi sahihi ya vielelezo vya elimu ya afya kwenye jamii na Taasisi.
i) Kumwalika Mdau na kumusikiliza au kutoa maelezo/ taarifa ya ziada juu ya vielelezo vilivyowasilishwa, vilivyopitiwa au kuhakikiwa kadri Kamati itakavyoona inafaa au kulingana na uhitaji.

SEHEMU YA NNE: VIKAO VYA KAMATI YA UHAKIKI WA VIELELEZO

4.1 Vikao vya Kawaida

a) Vikao vya kawaida vya uhakiki wa vielelezo vitakaa mara mbili kwa kila robo mwaka.

b) Sekretarieti itapanga tarehe ya vikao kwa kuandaa kalenda ya kila mwaka na itapitishwa na Mwenyekiti wa Kamati.

c) Taarifa ya tarehe ya kikao, agenda, pamoja na nakala za vielelezo vitakavyohakikiwa vitatumwa kwa wajumbe siku saba (7) kabla ya kikao.

d) Ili vielelezo vipitiwe kwenye kikao cha uhakiki ni lazima vielelezo viwe vimepokelewa na kuthibitishwa kupokelewa na Sekretarieti siku 15 kabla ya tarehe ya kikao. Hii itatoa fursa kwa sekretarieti kujiandaa na kuwapatia wajumbe muda wa kupitia au kuambatanisha nyaraka zinazokosekana kabla ya Kikao.

e) Kikao kitakuwa halali iwapo wajumbe saba (7) wa kudumu au zaidi watahudhuria

f) Taarifa kuhusu matokeo ya vielelezo vilivyohakikiwa itatolewa ndani ya siku kumi (10) za kazi baada ya uhakiki. Taarifa hizi zitawasilishwa kwa wateja kwa barua pepe au kwa nakala ngumu kwa kutumia hati ya kupokea au njia yoyote salama na haraka.

g) Vielelezo vitakavyopitiwa na Kamati ni vile tu ambavyo vimekidhi vigezo vilivyoainishwa katika masharti ya uwasilishaji (Checklist)

4.2 Vikao vya Dharura

a) Vikao vya dharura vitaitishwa iwapo kuna vielelezo vinavyohitajika kuhakikiwa kwa dharura
b) Mdau husika atapaswa kutuma maombi ya kikao. Kikao kitaitishwa baada ya muombaji kukubali na kukamilisha taratibu zinazoongoza kuitisha kikao cha dharura.
c) Taarifa ya matokeo ya vielelezo vilivyohakikiwa kwa dharura itatolewa ndani ya siku saba (7) za kazi tangu tarehe mteja alipokamilisha taratibu za maombi ya dharura.

4.3 Vikao vya Tathmini

Kutakuwa na vikao viwili kwa mwaka vitakavyopokea na kupitisha taarifa za robo mwaka kabla ya kuwasilishwa katika mamlaka husika.

a) Taarifa ya nusu mwaka ya uhakiki wa vielelezo itawasilishwa katika vikao vya Kamati ya Ushauri (Technical Advisory Committee).
b) Kikao cha pili cha Kamati kitajadili taarifa ya utekelezaji wa Kamati wa Mwaka mzima.

SEHEMU YA TANO: NYENZO NA GHARAMA ZA UHAKIKI WA VIELELEZO

5.1 Nyenzo ya kupitia na kuhakiki vielelezo

Vielelezo vya kuelimisha umma juu ya masuala ya afya vitapitiwa na kuhakikiwa kwa kutumia nyenzo maalumu. Nyenzo hiyo itahakiki vielelezo kwa kuzingatia mchakato wa uandaaji na ubora.

5.2 Gharama za vikao vya uhakiki

Gharama za uendeshaji wa shughuli za Kamati zitazingatia viwango vilivyoidhinishwa kwenye Mwongozo wa uchangiaji huduma wa Kitengo cha Elimu ya Afya kwa Umma.

SEHEMU YA SITA: HITIMISHO

Hadidu za Rejea za Kamati ya Uhakiki wa Vielelezo vya Elimu ya Afya kwa Umma zinafafanua mambo mbalimbali juu ya namna Kamati hii itakavyotekeleza majukumu yake ya kawaida. Mwongozo unataja Wajumbe wa Kamati katika makundi yao na namna wanavyopatikana, dhumuni na majukumu ya Kamati, utaratibu wa kuendesha vikao na shughuli za Kamati pamoja na nyenzo muhimu zitakazotumika katika kutekeleza majukumu ya Kamati. Pamoja nautaratibu uliowekwa na Mwongozo huu ili kuhakikisha ubora wa vielelezo, kamati itatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia sera, sheria, kanuni, taratibu, Miongozo pamoja na tamaduni za Kitanzania.

Kamati itahakikisha vielelezo vyote vitakavyopitiwa vinazingatia ubora wa aina ya elimu inayotolewa na walengwa wanaoelimishwa, muda na mazingira sahihi ili kufikia malengo yaliyokusudiwa. Vielelezo vitakavyopitishwa vitakua na lengo la kuelimisha jamii katika kujikinga na maradhi na kubadili tabia za wanajamii ili kutengeneza jamii yenye afya na kushiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo. Kamati hii itasimamia ubora wa elimu ya afya kwa kuzingatia maslahi ya Taifa.

MoHCDGEC-HPS-PRINTING PRESS DSM